Now, as regards running of state corporations, we find that the situation is pathetic in the sense that most of these are ran by the people who have retired. That means they have acquired a mandatory required at the age of 55 years. So, I don't understand how somebody who has served and then has retired, is now being made a chairman of such and such corporation, to be in charge. This is a situation where this fellow are just after serving the people who appointed them, they are told to sit there and eat well and feel probably better.

Now, the current constituion just comes from, I can call it nowhere, but Kenya should be this the president should be this So, in the case that we should have a preamble, we should have something say, something to about Kenya, something like that. Thank you very much.

**Com. Kangu:** Thank you , tupate Kenneth Wandera, ama utaki kusungumza?

**Mr. Kennedy Wandera:** Majina ni Kennedy Wandera, pendekezo langu la kwanza, ni viti vya ubunge vile vinavyo gawiwa kila mkoa, sababu ni kwa wakati huu tutaangalia Nairobi kuna wabunge wa 8, .....(Inaudible) North Eastern 11, Eastern 36, Central 29, Rift Valley 50, Western 24 na Nyanza 31. Mimi nilikuwa naonelea kila mkoa ugawiwe viti vya ubunge sawa sawa. Sababu sasa ukiangalia mtu akitoka Rift Valley, .....(Inaudible) Central tayari ashapata 50% ya wabunge, hapa nilikuwa naona, kila mkoa uwe na wabunge sawasawa,. Siyo wengine kumi kumi, wengine, sasa ukiangalia kama hapa Nambale, mbunge wetu ana division mbili ambayo anafanya kazi kubwa zaidi.

Ingingine ni kuhusu mambo ya urais, uraisi pale nikiguzia, mimi kweli .....(Inaudible) naongea hapa, lakini .....(Inaudible) ni ya serikali siyo ya rais. Sababu hata wakati huu Moi akitoka, mawaziri wake baada wataingia bungeni. Sasa mimi nilikuwa naonelea, Rais ajaye atakuwa mwaziri ambao si wa bunge. Sasa akienda mawaziri wake waende wote, mimi nikiingia na wangu, niingie na wageni. Sasa Moi akitoka Biwot anaingia, Okemo amengia, mimi nimengia, si tayari ufisadi uko, ni hayo asanteni.

**Com. Kangu:** Asante andikisha pale na sasa tupate Michael Owino, na kama hayuko, Hafas Ouma. Wewe ndiye unaitwa nani? Michael Owino Wafula.

**Mr. Michael Owino Wafula:** Kwa majina ninaitwa Michael Wafula, pendekezo langu ni hivi, kwangu sitakikuona serikali iwe ya mtu mmoja, kwa sababu, huyu mtu amepewa mamlaka mengi ama nyingi kuchaguwa kila kitu. Kando na hapo, msaada ukikuja unapitia office yake, ndiyo ufikie wengine. Hapao naona ni makosa.

La pili, kuna mtu anaitwa General Auditor, General Auditor, awe anachaguliwa na bunge, siyo mtu kwa sababu akifanya makosa, hawezi laumiwa.

La tatu, tukiwa na free education, iwe free education, siyo uwe free education ya kusema tu, iwe ya kusema iwe kwa vitendo. La nne au la tatu, central government and the local government iwe separate, isiwe pamoja kwa sababu central government inafaa isaidie local government.

La nne, askari akiwa ameandikwa, ameandikwa kulinda raia na mali yao, siyo kunyanyasa rai.

La tano, mwananchi awe uhuru kuongea, kutembea, ama kutibiwa hospitali. For example, mtu anaweza patikana hapa na accident, na naona wewe ni msamaria mwema unampeleka hospitali, kukifika kule utaambiwa, X-ray, 600/- corporate, sijuwi nini nini 600. Sasa kama wewe msamaria mwema, unaweza lipa hizo expenses kutoka wapi? Hapo mimi naona ni makosa.

La nne ama la tano la mwisho, tuko na watu wengine anaweza kukunyanyasa tu kwa sababu mtu mkubwa kwa office ni baba

yake ama mjomba wake. Sasa atakunyanyasa, baada ya kukunyanyasa atapiga simu. Asanteni kwa kunisikiza.

**Com. Kangu:** Na inaonekana kuna wengine waliandikisha majina mara mbili. Hakuna makosa, lakini makosa itakuwa wewe kutaka kuzungumza mara mbili. So, ukiwa umezungumza na tunakuita jina tena, utuambie nilikuwa nimeshazungumza, tupeane nafasi kwa mwingine. Nafikiria hayo tumeelewana, na haita rudiwa tena. Kwa sababu tunawona tumefanya hivyo na mtu mmoja ni hiyo ni makosa. Clevers Ouma, sawa sawa. Patrick Okochi. Geogrey Makokha, hayuko, Alfonse Okello, si wewe tulikusikiza, ama, okay, Zainabu Muyoti. Zainabu Muyoti, hayuko. Peter Mondo, amepeana, Matayo Nyegenye, hutaki kuzungumza? Umepeana, Syvester Muganda, hayuko? Fredrick Mugeni. Chrispinus Ondunga, Nabulinda Ooko.

**Councillor William Nabulindo:** Majina yangu ni Councillor William Nabulindo, kutoka Bukhaya West. Niko na memorandum lakini nitapitia maneno mawili matatu, halafu nipeane. La kwanza nitaongea kuhusu matibabu. Haya matibabu ambayo iko na cost sharing, nilikuwa napendekeza, hayo matibabu cost sharing itolewa kwa maana, kuna watu, ambao ni maskini hawa wezi kutibiwa, ni umefanya wengi wangekufia huko reserve kwa sababu hawawezi enda kwa matibabu, na tukifika kwa cost sharing, utakuta ule anafanya kazi na yale hafanyi kazi, na yale amekaa nyumbani wote wakienda watalipa pesa sawa sawa, kwa hivyo wale hawana pesa, huwa watu wao wanakufa sana. Mengine, mwenzangu alipitia ile ya macouncilor siwezi kupitia.

Inayofuata, ni wakati wa kupiga kura, kura zikipigwa zinataka zihesabiwe hapo hapo. Zisibebwe kwenda kuhesabiwa kwa station fulani, wapige kura, wanahesabu hapo, wanatangaza yule ameshinda. Na hiyo ikuwe kwa councilor na MP. Lakini ya president, ihesabiwe, pamoja yote kwa Kenya mzima apate 51%, ndiyo atangazwe mshindi.

Tatu, kazi inataka iwe shared among wakenya wote bila kabila. Utakuta kabila moja zimepata kazi nyingi na kabila zingine hazina kazi. Kwa hivyo, ningependekeza ikiwa inawezakena kupitia kwa katiba hii, waweke watu wapate kazi sawasawa. Na hata hapo, ikiwa ni elimu, utafika pale kwa mauniversities za Kenya, utakuta, sehemu zingine wanachukuwa kazi kama ya udakitari, inaenda sehemu zingine, engineering sehemu zingine, na sehemu zingine hutapata mtu, na wamepita mtihani sawa sawa.

Title deed kwa mashamba, tunataka zipeanwe kwa mwanakenya bure kwa maana, ile malipo ambayo iko kule ni nyingi, kwa hivyo ule ambaye ni maskini, hana pesa, anaweza kufa bila kupata titile deed, kwa maana hana uwezo.

**Com. Ayonga (Interjection):** Tafadhali tuliomba kutoka mwanzo kwamba, hatutaki makofi. Tunajua kwamba watu wanataka title deed, na hiyo ni point, imefanywa hapa na pale, si point ya hapa tu ya councilor, na kwa hivyo hapa hatuko katika mkutano wa siasa, ni mkutano wa katiba. Councilor endelea na umalize.

**Councillor William Nabulindo:** Na pia nikiguzia, wale ambao wenzangu waliongea juu ya pombe. Tukikaa hapa, tunaambiwa

pombe ya mrija imefungwa, lakini ukienda Nairobi unakuta wanapika pombe ya mrija, na iko licence. Kwa hivyo pia ningependekeza pombe ya mrija, kila area, hiyo pombe iendelea kwa maana ni pombe ambayo ilikuwa inasaidia wazee zamani kwa kuongea, na kupatia mawaidha, watoto wao wakiwe wanakaa pamoja. Na pia watu waliguzia hiyo chang'a wale waliguzia ni wengi. Sitaki kuguzia tena.

La mwisho, ni mambo ya Askari, kushika watu, unakuta askari anaenda kushika watu kwa pombe na amebeba bunduki. Lakini, akisikia mhalifu amepita, ukimwambia nauliza mwananchi, yeye bundiki yake ilikuwa na mlio aina gani? Na mnajuwa mwananchi hawezi kujua milio ya bundiki, kwa vile kufikia hapa, hiyo bunduki inaweza kwenda kushika watu wakifanya uhalifu, lakini pombe, iwe tu wanaenda kawaida kwa maana .....(Inaudible) nafikiria hiyo ndiyo ya mwisho.

**Com. Ayonga:** Asante, tumelewa, peleka hiyo kartasi yako ujiandikishe. Masiga J.

**Mr. Justus Masiga:** My names are Justus Masiga from around. My points are one, about our land system. For a very longtime, we have not had a well-defined system under which we have to subdivide our land. We have ended up having very small portions, which are not of any use. For example, if you have one acre currently and you have four sons, in the long run, how will you subdivide it? So, we need to have a well-defined system under which no more division of land can be done.

Secondly, Specialization: For a very long time, we have had that someone has been keeping one cow, and planting one acre of maize, then he is planting sorghum, so in th this has led to poverty, especially in our area, therefore, we need to have a system where each area is specialized in plants especially this is a sugarbelt region. We need to have come up with a system where we have to make sure that this area has all facilities where people have to grow sugarcane. But not keeping cows, millet and whatever.

Okay, there is an area where people plant maize, there is an area where people keep dairy cows not anybody doing whatever he pleases.

Lastly, Environment: Because of less specialiation, we have a system where,

**Com. Ayonga (Interjection):** Tafadhali, kule nyuma nasikia some grambling na huyu anaongea. Ningaliwaomba wale ambao pengine umechoka unataka ujinyooshe, unataka uoengee na fulani, mtoke kule nje mfanye hivyo, ili tumsikize huyu mzee. Endelea.

**Mr. Justus Masiga:** About specialization, we have had each and everybody is placing whatever he wants anywhere, especially, you get a chemical industry is placed in a residential place, and this is really happening in Nairobi and also around L. Victoria, you get, there is a factory that is trying to put the waste material into the lake and it is a fresh water lake. So, we need

to pump a system where everything is well defined. We need to have, if there is a trading zone, in a trading town, and if it is an industrial town, it is an industrial town, and if it is a service town is a service town.

And on environmental therefore, the government should come up with a system where we need to come up with a ministry of environment. Where, each and everybody can get some seedlings, something as somebody is over 18 years so that he can plant.

Then we have education, after 18 years, a citizen needs free education and medication. For cost sharing in hospital and schools have failed. Okay, there is something known as retirement benefit scheme, we have NSSF, okay those ones benefit those ones who are working. And those ones who have never worked in their lives how are they going to benefit from these things. We need to have a system where, each and everybody benefits from this country. We need to have elders homes that keep, like the old mama, that was have so that she can feel also at peace.

Okay, we have also this education system in our country, they are coming up with very shady private schools. If you get anywhere, even a grass thatched house, you get a private nursery school there. We need to have a law that defines these things.

Okay, we have also the issue of medical, any accident victim, is supposed to get free medical care up to the time he is recovers.

Then we have the passport issue, one passport is something like a needle in Kenya, to get it is just like a miracle. We need a system where all this passports should be issued at the district level. Thank you.

**Com. Ayonga:** That was now, Walter Odhiambo. Is there Odhiambo here? Okay, Odhiambo take a seat.

**Mayor Walter Odhiambo:** Mimi ni Walter Odhiambo, ningependa kutoa mapendekezo ya fuatayo kwa tume hii. Ningependa kutoa pendekezo la kwanza ya kwamba, wakati wa uchaguzi, kura zinapofanyika, ningependa tuwe na mtu ambaye anaweza kushikilia mamlaka ya serikali. Ambaye asiye mgombezi, wa kiti cha urais, mtu huyu, ningependa kupendekeza pengine awe kama speaker wa bunge, au chief Justice.

Halafu pendekezo, lingine, ni kwamba makamu wa Rais, Mayor na mwenye kiti wa county council, wawe wakichaguliwa moja kwa moja na wananchi, ili ya kwamba asipate kutumiwa vibaya.

Lingine, ni kupatana na presidential appointment. Hawo ni baraza la mawaziri, na makatibu wakuu, na viongozi wa mashirika ya serikali na mahakimu.



Hawo pia ningependa ya kwamba wakiwa appointed na the president, halafu, wawe wakilekwa katika bunge ili wapate kujadiliana na bunge, wakipitishwa, wawe appointed, na wakiwa rejected, watupuliwe mbali hivyo. Upane wa provincial administration, ningependa kutoa pendekezo ya kwamba machief na manaibu wao, wawe wakipata transfer mara kwa mara, ili pate kufanya hizo kazi zao katika sehemu kadhaa za serikali. Na mishahara yao, ipate kuangaliwa na wapewe mishara ya kutosha, ili wapate kutenda kazi zao vyema bila kuitaji hongo. Hayo ndiyo mapendekezo yangu.

**Com. Ayonga:** Bwana Odhiambo, next nataka William Masinde, amepeana. Daniel Omoro, yuko? Christopher Wandera, Isabella Nasonga. Isabella, huyo najuwa ni mwanamke. Isabella Nasonga, hapana, ikiwa alisha toa mambo yake. Wellington Nabulindo. Wewe ndiye Wellington. Okay, keti, chukua microphone. Na toa maoni yako.

**Mr. Wellington Nabulindo:** Mimi ni Wellington Odalo Nabulindo, maoni yangu ni sheria za barabara, kwa maana wako watu wanakaa karibu na barabara na wako na ng'ombe, gari ikikuja ikigonga ng'ombe, wewe utakimbia tu, kuona kwako utakimbia tu, lakini inatakikana mwenye gari lilo, ameona ng'ombe, na ng'ombe haina akili.

**Com. Ayonga:** Toa maoni yako.

**Mr. Wellington Nabulindo:** Maoni yangu mtu wa ng'ombe ndiye anatakikana alipwe, siyo mwenye gari kulipwa.

**Com. Ayonga:** Hilo ni oni lako moja, la pili?

**Mr. Wellington Nabulindo:** La pili, strikes kwa mashule, ukienda kwa shule, strike ikiwako, watoto ndiyo, wanaadhibiwa pekee yao, na inciters, hakuna mtu anapata makosa yoyote.

La tatu, sheria inatakikana askari akitembea, na bunduki kubwa, lazima awe na uniform, asiwe anatembea na bunduki kubwa na hana uniform.

**Speaker:** Na akiwa na bunduki ndogo?

**Mr. Wellington Nabulindo:** Akiwa na bunduki ndogo, pengine anaweza kuwa kwa kazi ingine tofauti. Lakini akiwa na bunduki kubwa na hana uniform hiyo ni makosa. Hayo ndiyo maoni yangu.

**Com. Ayonga:** Thank you very much. Bwana Nabulindo, hapo. Matayo Juma. Huyu Matayo, amatoa. Toa hiyo. George Oloo, ni wewe unaye kuja. Haya endelea kuja, halafu kuna Joseph Makokha, yuko, Makokha. Tena kuna Makoha mwingine anaitwa Alimida. Alimida yule tulisoma history, yuko wapi? Naye pia ni Makokha. Awe karibu. Endelea.

**Mr. George Oloo:** Mimi ni George Oloo, kiongozi wa waalimu katika kata ya Mundika. Nina haya ya kupendekeza kuhusu elimu. Napendekeza kwamba elimu iwe ya lazima kwa kila mtoto ambaye ana umri wa kuenda shuleni na iwe ya bure. Haitakuwa ya bure kwa maneno, lakini iwe kwa vitendo. Serikali iweze kuchunga pesa takriban, shillingi mia tano kwa kila mwanafunzi katika shule ya msingi,

**Com. Ayonga (Interjection):** Lakini point ni kwamba, compulsory free education. Sindiyo?

**Mr. George Oloo:** Hiyo ndiyo point.

**Com. Ayonga (Interjection):** Jinsi ambavyo serikali itafanya, hiyo tuiachie, endelea.

**Mr. George Oloo:** Pili, mayatima: Hawa lazima washugulikiwe kwa vyovyote vile waweze kupata elimu yao, kuanzia shule ya msingi, hadi kiwango chochote ambacho watafikia.

Mishahara ya waalimu, hasa katika shule za msingi. Ihalalishwe, yaani ifanyiwe harmony ili hayo marupurupu, yasiwe na kiwango kikubwa kama yalivyo sasa. Kwani utakuta kwamba wanafanya kazi sawa, lakini wengine wanapata marupurupu ya juu kuliko wengine.

Kukosa kazi, wale ambao hawaja ajiriwa, yafaa shirika fulani litengwe, na kila mwananchi wa Kenya ambaye amehitimu umri wa kupata kazi na amekosa kupata kazi, atengewe pesa fulani kila mwezi ambazo zinaweza kuendeleza maisha yake, angalau shillingi elfu moja kwenda juu.

Afya, inatakikana wananchi wa Kenya wapewe afya ya bure, bila kuhudimia.

Kuhusu rushwa, inatakikana kila mwananchi atangaze vile alipata mali, na iwapo hiyo mali itagunduliwa kwamba aliipata kwa njia ambayo haifai, ichukuliwe na serikali. Ama irudishiwe shirika ama sehemu ambayo hiyo mali ilitolewe.

Kishawishi ama tunzo, au zawadi, haifai kupewa na watumishi wa serikali wanapofanya kazi.

Uteuzi wa majudge ama chief justice, ufanywe na Rais, lakini bunge, lito uamuzi wa mwisho.

Kuhusu Ardhi, tuweke kiwango cha juu kama ekari 25 kwa kila mwananchi, hicho ndicho kiwango cha juu, iwapo utakuwa na zaidi ya hapo, utozwe ushuru.

Vinywaji vya kienyeji vihalalishwe. Tunajaribu kujidanyanya kwa sababu katika mabar yetu, tuna pombe ambayo tumeagiza kutoka ng'ambo, na hapa yetu ya kienyeji tunajaribu kuua.

Umri wa Rais uwe kati ya miaka 35 hadi 75. Na Rais asiwe mbunge.

Vyama vya kisiasa viwe vitatu. Vipunguzwe na viwe vitatu. Msimamizi ama mzee wa kijiji apewe marupurupu na serikali.

Mahari ilipwe ikiwa mtu yuko hai. Na iwapo moja atafariki, mahari iondolewe. Asanteni.

**Com. Ayonga (Interjection):** Thank you so much, unaweza kwend kule ujiandikishe. Wewe ulikuwa George Oloo. Wale wa Makokha wawili wajaonekana? Gilbert Nderia au Maderia. Jackson Ogolla, kuja mbele. Halafu David Masinde uwe karibu, endelea, chukua microphone sema majina yako.

**Mr. Jackson Ogolla:** Mimi kwa majina naitwa Jackson Ogolla, mimi ni mkulima. Naona kwa maoni yangu, huu udongo wetu imekuwa mbaya sana, babu zetu walianza, huu udongo wetu tumesha tumia lakini sasa isha haribika, sisi ni wakulima. Vile tumeenza kulima, tunatumia kununua mbolea, tunatumia lakini tukipenda, hatupati mazao vile inavyofaa tupate, hata tukipata mazao yenyewe, market hatuna,

**Com. Ayonga (Interjection):** Kwa hivyo unatakaje, maoni yako?

**Mr. Jackson Ogolla:** Maoni yangu mimi naona, watuletee factory karibu, ile ambayo tunaweza tupate huko kazi tuandikiwe, tusije tukaenda mbali kutafuta kazi. La pili, mimi naona upande wa president, sisi wana raia, tumekaa huku reserve watu wengi sana, wenye hatuna, kwanza hatutoi maoni, lakini vile mumekuja kuaribu sasa, tumefurahi sana. Sisi wana raia ndiyo, tunapiga kura nyingi sana, na hizo kura zetu kwa wananunua kwa pesa, hata hivi karibuni wata tuletea, saa zingine shilingi hamsini hamsini, kutudanganya. Hata thumni. Lakini kwa hivyo sasa, tunataka watuletee kitu cha ukweli. Hii majuzi walisema watatuletea factory ya miwa. Hatujai pata, wanaimba tu.

Mambo ya ukimwi, ukimwi wafanyi kazi wa serikali wenye wanapata pesa, ndiyo wanasambaza ukimwi sana. Kwa hivyo sisi, wenye hatuna pesa, hatuwezi sambaza ukimwi, ndiyo utapata mfanyikazi wa serikali ako na pesa, halafu anadanganya mtu ...

**Com. Ayonga (Interjection):** Kwa hivyo ni bahati kutokuwa na pesa? Jinsi watu waliyo na faida ni wale hawana pesa. Na wale walio na pesa, ukimwi itachukuwa. Basi endelea, oni lako la mwisho.

**Mr. Jackson Ogolla:** Oni langu la mwisho, inafaa wafanyi kazi wa serikali, wawe, kuna mtu mmoja anayeweza kupata saa ingine mishahara ya wengine, mishahara ya wengine hata 35, na mimi hapa hata sina mishahara wowote. Afadhali hata mtu, huyo

mtu apate tu mshahara wake mmoja ule ambao alisomea kazi yake. Asije akajibandika kazi nyingi na ile hata haja somea, wanambandika tu,

**Com. Ayonga (Interjection):** Asante sana Bwana Ogolla. Ende kule ujiandikishe, nataka David Masinde, Masinde yuko wapi? Johna Odour, John Oduor. Ndiye huyo, anafuatwa na Dismus Musumba, Dismus Musumba uko? Hebu kaa karibu tukuone, asante, wewe endelea, songa hapa ukalie hii bench hapa.

**Mr. John Oduor:** Mr. John Oduori, mimi ningependa kuchangia kidogo kuhusu huu mjadala. Yangu yatakuwa mafupi na mengine nitapeleka kule. Naongea kuhusu askari, askari wasienda kuwashika mtu yeyete usiku bila liguru, kwa maana hii inafanya wezi kuvaa uniform na kudanganya ya kwamba ni maasikari, unapo funguwa milango, wanakaribia. Hatuwezi kutofautisha askari na mwizi usiku bila liguru.

La pili, case za mashamba, case za mashamba ziwachiwe liguru, assistant chiefs na chiefs kwa maana hao wanajua, fulani alikuwa akiishi namna gani, hata kama kuna mzozo, kuliko advocate, na judge ambaye hajui vile hawa watu walikuwa wanaishi.

Ningependelea pia, liguru apewe mshahara kutoka kwa serikkali, kwa maana nikichunguza, maligurus wanafanya kazi nzito sana, hata kama hii ambayo ninawapatia saa hii ya kusema wewe wakitembea na askari, usiku ikiwa kutakuwa na lazima askari kushika mtu usiku. Hiyo itataka wao wakipata kitu kidogo, na kutoka kwa serikali.

Pia ningeonaa, hata kama assistant chief angetolewa, liguru awe mtu wa kwanza halafu chief. Kwa maana hii chief na sub chief, ni kama wanafanya kazi moja tu. Unaweza enda office ya chief utapata sub chief ndiye, chief hayuko, hiyo mshahara ingine inaenda bure, mtu mmoja atolewe. Hiyo pesa irudi kwa liguru ambaye anafanya kazi nzito bila pesa. Yangu ni haya, mengine nitapeleka kule, asanteni.

**Com. Ayonga (Interjection):** Haya nenda kule uweke sahihi Dismus Musumba,

**Mr. Dismus Musumba:** *Elira nangwa dismus musumba.*

**Translator:** He is known by the names, Mzee Dismus Musumba.

**Mr. Dismus Musumba:** Mimi nauliza, nikiwa mgonjwa niende hospitali, nitibiwe bure, bila malipa.

**Com. Ayonga:** Inaudible.

**Mr. Dismus Musumba:** B, tukipigana watu wawili, na mwingine akiniumiza, nipelekwe hospitali na pesa, tena kama mimi nakufa huko, nirudishwe na pesa za serikali. Ni hayo tu.

**Com. Ayonga:** Enda kule mzee ujiandikishe. Kuna mama anaitwa Florence Nakhulo. Alimaliza, kuna Fred Wesonga. Kuna Clement Ouma, haya...

**Mr. Clement Ouma:** Kwa majina ni Clement Ouma. Mimi napendekeza ya kwamba, wafanya kazi wa serikali wote, wawe wakipigwa transfer mara kwa mara.

Ya pili, mtu yeyote ambaye anaitwa mfisadi, asitolewe bond, akisha gunduliwa, akae ndani mpaka afanye case, akashinda ndiyo awachiliwe.

Jambo lingine, mbegu za wakulima, wakitaka rahisisha mkulima mdogo pia afaidike, wafanye bei ya mbegu, mbolea iwe chini.

Neno lingine, mimi naonelea ya kwamba, serikali ina sheria ingine ambayo inaumiza raia, mtu akigongwa na gari hapa njiani, anachukuliwa bure, akisha pelekwa kwa postmortem, hospitali, wanataka wenye mtu waende wachukuwe, na hawana hata vitu. Huyu mtu si ataozea huko.

**Com. Ayonga:** Kwa hivyo unataka aje?

**Mr. Clement Ouma:** Nataka serikali ikichukuwa, irudishe tena.

**Com. Ayonga:** Okay,

**Mr. Clement Ouma:** Jambo lingine, kuna watu ambao wanafanya kazi kama maliguru, sub chief, machief, wawe wakipewa transfer pia. Kwa sababu wana hatred pahali pengine kwa wale wa ukoo wao hapo, wanawatumia kwa njia ya kimila mbaya, wana wa hate. Wawe wakipelekwa transfer pia.

**Com. Ayonga:** Okay, yamwisho?

**Mr. Clement Ouma:** Ya mwisho mimi nasema, watu watibiwe bure kwa ma hospitali kwa sababu, zamani tulikuwa tuna lipa pesa kidogo kwa serikali, ile inaitwa tax na tuna tibiwa bure. Na saa hii hata mtu akiwa na mimba, nalipa tax ya mimba hake hiyo,

**Com. Ayonga:** Ndiyo,

**Mr. Clement Ouma:** Lakini sisi sasa tulipa deposit sharing.

**Com. Ayonga:** Lakini si mzee umesema, ume - recommend free medical treatment. Hiyo ndiyo point?

**Mr. Clement Ouma:** Yaah, maoni yangu yameishia hapo.

**Com. Ayonga:** Na sisi pia tunasema uende kule, ueke kidole. Wewe ni? Ndubi Titus, ngoja kwanza, huyu anaye itwa Enos Ouma, wewe ulikuwa unafwata Enos Ouma. We Enos kuja, halafu Ndubi kaa hapa karibu, huyu akimaliza uanze. Usiende mbali Ndubi.

**Mr. Enos Ouma:** Kwa majina ni Enos Ouma, kutoka Buyama Sub Location, Nasewa Location. Nitaongea kwanza nitatangulia na serikali za wilaya. Kuhusu leseni ambazo zinatolewa na county council. Mimi nikiwa mwana juwa kali ambaye ni seremala, tunapenda zaidi kufanya hii kazi kuendeleza taifa letu, lakini kuhusu leseni, napendekeza, serikali imeweka kiwango cha juu mno. Na tena la pili, leseni hii, kwa mfano ikikata mwezi wa sita tarehe moja, ende hadi tarehe sita mwezi wa kwanza mwaka ujao, iwe ikimaliza mwaka mzima.

La pili, kuhusu primary text books, na secondary text books, vitabu hivi, viwe ni kwamba, hata kwa mfano shule hii ya Lwanya, vitabu ambavyo vinapatikana katika shule hii, hata ukienda kule Nairobi, viwe ni hivyo hivyo, bila kubadilisha leo ni hivi, kesho, ni hivi vitabu, ni vingine, sasa hii imekuwa taabu kwa wazazi kuweza kumudu madiliko ya kila mara ama kila mwaka.

La tatu, kuhusu, matangazo ya leo katika bunge. Napendekeza ya kwamba, taarifa hii iwe ikizikizwa moja kwa moja mara tu, mbunge ama yeyote aliye bungeni, anapongea. Iwe hewani, katika radio na katika vyombo vya television.

La nne, kuhusu elimu ya watu wazima: Nangependekeza serikali yetue ya Kenya ichukuwe mfano wa Uganda. Kwa mfano mtu amesoma, na amefikia darasa la saba, na kwa bahati mbaya cheti chake kikapotea, pengine alifanya KCPE, na cheti kikapotea ama kikateketea ndani ya nyumba. Sasa napendekeza, huyu mtu, ajiandikishe upia, ajiandikishe kama private candidate, katika shule, na aruhusiwe kufanya mtihani huu, hata iwapo yeye ni mzee.

La tano, kuhusu provincial administration. Ingawa hili limesemwa, lakini ni tofauti tu kidogo, na yangu. Watawala hawa, wawe wakihamishwa hapa na pale, lakini katika division yao.

La sita na la mwisho, budget bungeni, iwe ikitayarishwa na wabunge kwa jumla siyo tu mawaziri pekee.

**Com. Ayonga:** Thank you, hebu niwambie wale ambao mumbaki, tafadhali msirudie yale ambayo yamesemwa, kama mtu amesema, jambo ambalo ulitaka kusema, wewe sema, ninaliunga mkono, na kutoendelea ili tupate nafasi ya wengine kusema. Sasa wewe ni .

**Mr. Titus Ndubi:** My name is Titus Ndubi, Treasurer KNUT Busia branch.

Agriculture: Kenya is an agricultural country, and the farmers in this country need to be empowered. For that I propose that one, we should have a farmers bank, where farmers can get money to develop their farms.

Two: The government should help farmers market their products.

Then incentives, should also be extended to the same farmers, so that it is easy for them to produce the necessary or the said products.

Trade Unionism: Kenya is a signatory to the international labour organization Charter or convention, and as a result therefore, we should make compulsory, that all workers in this country belong to one trade union or the other. It is a basic right and as we have seen of late, there has been this retrenchment being conducted left and right, and the number of citizens have been victims of very awkward situations.

For the Kenyans who are not yet employed particularly the already the graduated group, I propose that the government should provide an upkeep that is, at least they get something at the end of the month because they know, that a number of them are family men, and given the style of life today, like for example malaria, it attacks a member of your family, it is possible that somebody will use life simply because you cannot afford maybe twenty shillings with which, you can buy some tablets for treating malaria.

On education, I propose, that basic education starting right away from pre-primary, up to class 8 should be free, compulsory and universal. Along with that also, computer studies or literacy, should be made mandatory and tested be at all level of the education curriculum or cycle.

Then parliament, should not be empowered to ammend laws of the constitution, there should be a refrundum, for, power should be given to people.

The president should not be the vice chancellor of any of the public universities. If anything, we have some reknown scholars who actually could act as role models, to inspire the would be students for the same. While there, I propose also, that the academic qualifications for anybody to contest for presidency should be form four and above.

**Com. Ayonga:** Ndubi time inakwenda yako.

**Mr. Titus Ndubi:** Yaah,

**Com. Ayonga:** Hakuna?

**Mr. Titus Ndubi:** Liko. While there are also, the president, for misconduct should be impeached.

While also, for MPs, if for example there is persistence, lack of quorum whereby a particular MP is not very keen at attending parliament, he should also be recalled.

Then, instead of having the Attorney General attending parliament, every day, he should be left to sit at his desk and do his job and instead we should have a minister for constitutional affairs doing the same.

People in essential service area, like the teachers, the police, the medical group, should be well remunerated so as to encourage them to perform well. Thank you very much.

**Com. Ayonga:** Thank you, nenda huko ujiandikishe. Kuna Chrispin Makokha. Si huyu tulimsikia? Yuko wapi? Halafu atafuatwa na Pascal walumbe, yuko wapi? Okay, uwe karibu hapo. Dakika tatu tu.

**Mr. Chripinus Makokha:** Jina langu ni Chrispinus Makokha, kuna maneno ambayo nilikuwa nimeendika lakini yamesemwa mengi. Kwa hivyo, nitasema tu machache.

Number one: Kwa upande wa utawala, napendelea serikali ya majimbo, kwa maana serikali kuu imeshindwa hata kumanage Nairobi. Na imekusanya vitu zote Nairobi. Na watu wengine hapa chini wanakufa njaa. Ukiingiak kule Nairobi hata stage pekee yake ni mbaya. Na president ako pale karibu na vitu vingine. Nataka serikali ya majimbo hapa, na hawa watu wawe wakichaguliwa na wananchi moja moja, kutoka kwa governor mpaka kwa liguru. Na wote walipwe mshahara na serikali. Na tukiwa na hiyo serikali ya majimbo, hata viwanda vitakuwa hapa chini. Kila kitu kikiwa hapa chini, sisi sote tutaandikwa kazi, hatutakuwa na shida. Hilo lilikuwa neno langu la number one.

Number mbili liko kwa basic rights, kwa basic rights nasema hivi, ninapendekeza tangu nilipokuwa hapa, sijasikia mtu akiongea, juu ya neno fulani, nalo ni ukimwi. Mtu anapozaliwa, anazaliwa kuishi, na kuna watu wengine wana viini hatari vya ukimwi. Na kazi yao ni kutembea tembea wakiwa wengine, kwa hivyo napendekeza ya kwamba, katika katiba mpya, serikali ifanye uchunguzi kwa watu wote, yeyote anayepatikana na ukimwi, yeye na bibi yake, wawekwe mahali. Serikali ijenge mahali wawekwe huko, badala ya kuendelea kuwa watu wengine. Ikiwa nimezaliwa kuishi, na wawe unatembea tembea na ukimwi, kupatia mimi unaniua, na watoto wake wale wamebaki, serikali ichukuwe isomeshe. Pesa nyingi ambazo inachukua kwenda kusema ati wana advice watu kwa ukimwi, hiyo pesa itumike kusomesha watoto polepole.



Jambo la tatu ni kwamba hapa Kenya, kuna makabila mengi na haya makablila mengine wanasema watoto ni wa wanawake, na wengine wanasema watoto ni wa wanumme, sisi waluhya watoto in wa wanumme, napendekeza katika katiba, mtoto yeyote, ambaye amezaliwa katika nchi hii ya Kenya, awe mtoto wa mwanaume. Mwanaume ndiye alitoa mbegu ile kubwa, siku hizi ukiweka chakula yako kwa stove,

**Com. Ayonga:** Maneno ya siku hizi, wewe umesema watot wote wawe wa wanaume, hayao ni maoni yako, endelea.

**Mr. Chripinus Makokha:** Nimemaliza hapo. Nilikuwa tu nataka kusema maneno matatu, na hayo matatu nimemaliza. Asante sana.

**Com. Ayonga:** Asante, enda huko utoe hiyo karatasi. Sema mjina yako na endelea.

**Mr. Pascal Walumbe:** Mwenye kiti, tumefurahi sana kwa kuja kwenu. Niko na maneno mawili tayari mengi imeshasemwa hakuna nafasi ya ku...

**Speaker:** Majina.

**Mr. Pascal Walumbe:** Majina ni Pascal Walumbe, kutoka Nang'oma Location. Nitaongea kwa upande wa mazingira, na mali ya asili. Maswala ya mazingira, ambayo yanapaswa kuingizwa kwenye katiba iwe misitu, mito milima, madeni, na wanyama wa pori. Serikali inapaswa kuwa na uwezo wa kulinda mazingira katika katiba.

Mali ya asili, imilikiwe na serikali.

Jamii ihusishwe katika usimamizi na ufadhili wa mazingira.

Mali ya asili, isiharibiwe na jamii.

La mwisho mwenye kiti, tunaomba ma chief, manaibu wa machief, na ligurus, yaani waze wa kijiji, wapewe uwezo kabisa, wa kuaambia wanakenya katika sehemu zao, amri za serikali na sheria, na katiba yetu, waende kama wanawasomesha. Wapewe pia uwezo wa kushugulikia mambo ya mashamba kati ya jamii katika vijji vyao. Tunaomba pia maliguru, na waze wa vijiji, serikali iwe iwalipa allowance kidogo kidogo, hata ikiwa ni shilingi mia moja kwa mwezi, shauri kazi yao ni muhimu sana kwa serikali.

Tunaomba pia wazee, warudishiwe utamaduni wao wa zamani, jamii kukaa pamoja jioni, baada ya kazi yao mashambani, na kunyua pombe yao ya murija, *amalwa*. Wakiongea mambo ya maandeleo na watoto wao.

Mwisho tunaishukuru kamati hii ya CKRC kwa kazi yenu mzuri, mungu awalinde. Thank you very much.

**Com. Ayonga:** Sasa wewe nenda uweke kidole. Mzee, upande huu, wacha kuangalia watu huko. Kwenda hapa. Karuri Wawire yuko wapi. Ndiye huyo, halafu kuna huyu Rachel Amoti, alikwisha sema.

**Mr. Karuri Wawire:** Mimi naita Karuri aiwe kutoka katika Mundika Sub Location. Maoni yangu ni machache, na jambo la kwanza, ambalo nitasema ni kuhusu administration. Administration wakuwe chini ya sub chief na chief na Liguru. Wasiwe watu wa kutanga tanga katika maboma ya watu, unakuta mtu umekaa, unamambo yako ambayo unazungumza na watoto wako, wamekuingilia, mzee unafanya nini? Hatutaki hiyo katika katiba mpya.

**Speaker:** Inaudible.

**Mr. Karuri Wawire:** Yaah, mimi nakaa, unakaa na watoto wako mnazungumza, na hawa wakiingia wanakuuliza mzee unafanya nini. Sasa unashindwa.

**Com. Ayonga:** Endelea.

**Mr. Wawire:** Pili, katika sheria yetu, ya Kenya, sheria ambayo tutataka itolewe, askari akikukuta na makosa, mfanye naye case tu siokwenda kwa kortini na kuambiwa, ati umepatikana na gunia la bangi, na kumbe siyo wewe ambaye umepatikana, na hilo , gunia, sababu unaweza kuwa uko katika shamba na mhalifu wa hiyo bangi, atapita hapo, akiangusha hapo, police administration anamfuata, sasa wewe ndiye utakuwa unashugulikiwa hiyo. Na siyo wewe mwenyewe.

**Com. Ayonga:** Kwa hivyo unataka ifanywe aje?

**Mr. Karuri Wawire:** Akiwa amekukuta na hiyo, mfanye case pamoja naye. Bali siyo kuitishwa tu ati nilisikia .

**Com. Ayonga:** Okay, na point ingine?

**Mr. Karuri Wawire:** La tatu limesha zungumzwa na wengi kuhusu ma liguru wapewe kitu kidogo, na uchunguzi wa mashamba. Hawo ndio wanajuwa vile watu wamezaliwa na vile wamekaa. Siyo kwamba, koti itatambua. Mkisii atakuja kuamua shamba la Busia naman gani? Hawezi, hiyo ni unyanyasaji. Hiyo sheria itolewe. Ndiyo hayo tu.

**Com. Ayonga:** Okay, asante sana. Nenda huko ujiandikishe. Wapi yule Wawire? Robert Apai, yuko? Wewe ni nani. Okay,

endelea.

**Mr. Rober Apai:** Mambo mengi watu wamesema,

**Com. Ayonga:** Sema majina yako.

**Mr. Rober Apai:** Kwa majina naitwa Robert Apai.

**Com. Ayonga:** Sema yale hayajasemwa.

**Mr. Rober Apai:** Isipokuwa nitaeleza mambo mawili, matatu. Jambo la kwanza nilikuwa napendekeza sub chief aondolewe. Tubakie na liguru ambaye ndiye mzee wa mtaa.

Jambo la pili nilikuwa napendekeza , DO aondolewe. Kwa sababu unaenda kwa office hayuko. Tubakie na chief. PC naye unaweza kufa bila kumuona, naye aondolewe.

Jambo, lingine nilikuwa nasema, mtu yeyote akifungua biashara hapa Kenya kama kiwanda, serikali imulipishe ushuru fulani ili akinyanya sa huyo mafanya kazi, watoe hizo pesa ambazo aliwalipisha hiyo, walipe huyo mfanyi kazi.

**Com. Ayonga:** Inaudible.

**Mr. Rober Apai:** Nilikuw naongezea jambo lingine moja.

**Com. Ayonga:** Hebu tupate hilo moja

**Mr. Rober Apai:** Jambo lingine nilikuwa nasema, kila mtu awe na uhuru wa kuongea mahali popote.

**Com. Ayonga:** Asante, uende huko ujiandikishe. Pelicas Wanjala. ...Inaudible.

**Mr. Pelicas Wanjala:** Majina yangu ni Pelicas Wanjala. Basi maoni yangu ni hii, hapa katika Busia, kuna wezi zaidi wa mifugo, lakini serikali nayo haitusaidii. Na bado kuleta mbwa mahali ambapo wale walioiba yaani mahali pa zizi, na kuleta ile picha ambayo wanapiga, ambapo watu walikuwa wanang'ang'ania, machine hizi hikiharibika ama vipi?.

Habari ya ugojwa, watu wamesema hapa ukimwi nini nini, lakini njia ya uimwi ni njia ambayo imekuwa ngumu. Ikiwa kama mtu wa daktari amesha nipa watu hawa wana ukimwi, wasitengewe kambi yao,



hivyo sisi haya mambo yanatuambua sana.

**Speaker:** Inaudible

**Mr. Pelical Wanjala:** Na mimea hii kama tulivyo peleka, inataka tusome kulima au namna gani? Sasa hii mambo inaweza kutuudhi sana. Sasa hapa tulikuwa tunalima pamba, tulikuwa tunapata pesa zaidi. Sasa pamba tunalia, na mahali ambapo tunapeleka hakuna. Je, ni mimea gani ambayo tunaweza kupata ili tujipatie pesa. Hayo ni yangu tu.

**Com. Nunow:** Asante sana mzee Wanjala, tafadhali njoo pale ujiandikishe, uje hapa mbele tu hapa mbele. Kuja mbele utangulie wengine. Mohamed Wandera, endelea.

**Mr. Mohammed Wandera:** Kwa majina naitwa Mohamed Wandera. Maoni yangu, nataka liguru apewe mamlaka zaidi, awe mtu mwenye amesoma, at least awe na primary education. Awe na certificate, achaguliwe na raia kwa kipindi cha miaka mitano kwa njia ya kura.

Aanzie umri wa miaka 35 na asiwe zaidi ya miaka 65.

Apate mshahara usio chini ya elfu sita.

Upande wa Administration Police: Ningependekeza, wasiweze kuingia katika area ya liguru, bila yeye kujua, wapate idhini kutoka kwa liguru, ndipo wafanye msako au wamshike mtu. Katika hiyo, hiyo ofisi ya liguru, kuwe na local council, ambayo itajumuisha idara kama ya usalama, elimu, maji, information, health na agriculture. Ili kufanya ofisi ya liguru kuhudumia ipasavyo.

Assistant chiefs ningependekeza aondolewe, ili liguru atawale area ya assistant chief.

Agriculture department: Itoe mbegu kwa raia kwa njia ya loan pamoja na kutoa ushauri kwa raia, kwa njia ya kupanda mimea mbalimbali, kwa njia ya kitalaam. Vile vile, idara ya agriculture ifungue ama ianzishe taasisi ya kutoa mikopo kwa wananchi, ili wapate nguvu kamili ya kuendeleza kilimo. Taasisi hizo ziwekwe kwa kila location.

Upande wa accident: Raia anapogongwa na gari ama anapouliwa na gari katika barabara, kwa bahati mbaya raia agongwe na gari barabarani, yule aliye mgonga, apewe jukumu la kugharamia mazishi ya huyo aliyeuliwa, kumpeleka mortuary, kumrudisha, na kugaramia mazishi, ya hiyo maiti. Ni hayo tu, asante.

**Com. Nunow:** Asante sana Bwana Wandera, tafadhali jandikishe hapo. Geoffrey Magoba. Michael Yinda, David Wawire, uko? Na .....(Inaudible) Philip nani? Okay, imeandikwa vibaya, lakini hivyo, sawa, utamfuata.

**Mr. David Wawire:** Kwa majina mimi ni David Wawire. Mimi nilikuwa na mapendekezo kama nane, tisa namna hii, lakini watu walizungumza mengine, na nitafupisha mengine.

Mimi, upande wa council, pendekezo langu, kwa sheria ambayo najuwa hii ni amendment, ambayo hawakuvunja zote, lakini sheria ya council kuwa peke yake, katika Kenya councils zote, mimi ninaonelea councils zirudi kwa Central Government, kama nchi zingine. Kwa sababu sisi ambao tuko hapa mpakani, na waganda, waganda local government imeenda kwa central government. Kupunguza shida, kwa sababu nina zungumza kama mfanyi kazi ambaye nime retire katika council. Miaka ya zamani, council ilikuwa ikiunganishwa na waalimu, na veterinary department, na hata na idhara zingine, ukosefu wa kulipa mishahara ya wafanyi kazi haikuweco, kwa hivyo ndiyo mimi napendeka kw sababu saa hizi, tunachanga pesa kutoka kwa wananchi, haitoshelezi, mahitaji ya council, na inafanya councillors peke yao ndio wanalipwa, na wafanyi kazi, are not getting any salaries at all. Kwa hivyo, maoni yangu ilikuwa, iende central government kwa sababu minister wa local government analipwa na cental government. Hiyo ni kuongeza hapo.

Mashamba: Tulipo kuwa katika ukoloni, tuliambiwa mashamba, tuling'ang'ania uhuru tukisema tukisema mashamba tutapewa, na if somebody has retired, a high rank, anapewa shamba bure. Na sisi local people, tunapata taabu, when we are talking of this amendment, we are talking in Kenya, we are not talking in Busia. Tukizungumza kama Busia, tutakuwa hatupangi sheria hizo sawa sawa. Mashamba hii, igawiwe watu wote. Kwa sababu, wewe ukimpa mtu asante, ati anafanya kazi kwa serikali vizuri, mbona mimi amabye sikufanya kazi kwa serikali nitapewa nini? Kwa hivyo sheria iwekwe mashamba hii, wapunguze, kumpa mtu mmoja acre mia mbili, au acre mia tatu, au elfu moja na mia tatu au elfu moja na mia tano, sheria iwe, mtu awe anapata acre kulingana, kwa sababu anaweka zingine nyumbani kwake. Sasa akipewa, apewe kama acre kumi, hata kumi na tano, ili watu wengine nao wapate.

Elimu: Elimu, kwa upande wa u - councilor, elimu, uongozi ni kipawa cha mtu kutoka kwa mungu. Elimu mtu aanzi darasa la nane, kwa sababu hata waongozi wengi ambao wako saa hizi ambao wanasema wanatak kustaafu, walikuwa watu wa darasa la nane, mimi nimeonelea watu wote waanzie darasa la nane na kufikia hata kama mtu ana degree, wale ambao wanaleta uchumi kukosa, ni wale amboa wako na degree.

Security: Sisi katika Kenya, movement yetu ni mbaya sana. Na nimeonelea hiyo movement ya security, ukitoka for example, Busia, unataka kuenda Nairobi, kama security inaweza kuwa arobaine njiani, which means, the first the security you started, was not trusted. Serikali ikiona mtu anatoka Busia anafika Bumala, ndiyo anakamatwa, si yule ambaye alianzisha security afutwe kazi? Sababu, nimeona watu wanasema bangi, nini, nini, lakini security ndiyo imekuwa anachukuwa hapa, unatoka hapa unacheikiwa hapa, the same vehicle. Kwa hivyo, hii security tumeona, kama wale watu ambao wamekuja kulinda security, na hii amendment tunaweka, mimi naonelea, sheria ya zamani ya wakoloni ni sawa tu. Lakini, mwenye kulinda sheria ndiye hakuna.

**Election:** President awe MP ua minister au parliament. Sisi ndiyo tuliwachaguwa, nowadays, ninaona, mnasema tutunge sheria, na sheria kama wewe umechaguliwa rudi kwa wale watu walikuchaguwa kwanza uniambie sisi tunataka kuchaguwa huyu, mimi nimeona sisi raia mtuache sisi tutachaguwa president, sisi wenyewe. Kwa sababu ndiyo sheri ya zamani. Tulikuwa tunachaguwa president sisi wenyewe. Ni mikoa tu kusema, tumependekeza, lakini siyo minister mmoja kusema yeye ndiye anapendekeza. Akipendekeza, he is making us to run in another way which is not good. Hiyo ni election.

**Transporting:** Mimi niko hapa Busia, niko mpakani, transporting, mimi naenda Uganda, nina nunua chakula, sababu sisi tuko na ukosefu wa chakula, hakuna security yeyote mtu anakwambia, wale kitu wanataka ni pesa, lakini ukikuja Kenya, unaambiwa unatoa hii mahindi wapi? Wewe unatoa wapi? Fungua, when you have no food and your security says you should not move with this food. Do you want us to throw where, mimi nimeona transporting of goods ni mbaya sana. Ijapo kuwa , Rift Valley peke yake, ndiyo movement inakuwa sawa. Kwa hivyo sheria hii, tunaiweka tu kwa Rift valley, na area zingine si za Kenya. Kama ni za Kenya, kila mtu a transport mali yake freely.

**Rasilmali:** Mimi nimekaliwa 1940, ni nime zaliwa hapa Kenya. Katika 1940, na nimeenda sasa niko na miaka 60, rasilmali ile inanzia tu Kisumu, Rift Valley, Nakuru, Eldoret, Nairobi, Mombasa, sasa tuache serikali ya Kenya katika Matayos ni hizo peke yake, na kama ni sheria, ati tunataka ifuatwe, kila watu wapate rasilmali sawa.

**Com. Nunow:** Ya mwisho.

**Mr. David Wawire:** Mimi nimeona hayo machache, pengine wengi walisema, lakini mimi nilirudia kwa sababu wengi hakuwa wanatoa comments. Lakini mimi naona ni comment kwa sababu, sisi tuko Kenya. Hatuezi kuzungumza maneno ya Busia, we are not Busia, we are not making the law, we are making the law for the whole Kenya, we are not only for Busia. Thank you very much.

**Com. Ayonga:** Thank you very much Bwana Wawire, tafadhali utaandikisha pale, Philip Boi, tafadhali jarivu kuzungumzia zile points hazikuzungumziwa kusudi, itakuwa maoni ya constituency hii yakiwekwa yote pamoja.

